

Changamoto Zinazoathiri Matumizi ya Filamu za Kibongo zenyne Tafsiri katika Ufundishaji wa Msamiati wa Kiswahili kwa Wageni

*Julius Matovu na Pendo Salu Malangwa
Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, UDSM*

Ikisiri

Makala haya yamechunguza changamoto zinazoathiri matumizi ya filamu za Kibongo zenyne tafsiri katika ufundishaji wa msamiati wa Kiswahili kwa wageni nchini Tanzania. Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Ujifunzaji kwa njia ya Media Anuwai ya Mayer (2009). Uchambuzi wa data za utafiti huu umetumia mkabala wa kitaamuli na mbinu ya kuchambua maudhui. Data za utafiti huu zilipatikana kutoka katika vituo vitatu vinavyofundisha Kiswahili kwa wageni ambavyo ni Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Kiswahili na Utamaduni (KIU) na Kituo cha Mafunzo ya Ushirikiano na Maendeleo ya Kimataifa (MS-TCDC). Data za makala haya ni sehemu ya data zilizokusanywa kwa ajili ya shahada ya umahiri¹ ya mwandishi wa makala haya akishirikiana na msimamizi wake ambaye ni mwandishi mwenza wa makala haya. Mbinu za usaili na ushuhudiaji zilitumika kukusanya data kutoka kwa walimu tisa wanaofundisha Kiswahili kwa wageni. Matokeo ya utafiti huu yameonesha changamoto mbalimbali zinazoathiri matumizi ya filamu za Kibongo zenyne tafsiri katika ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni. Changamoto hizo ni pamoja na ukosefu wa vitendeakazi, filamu kuchukua muda mwingi wa kipindi, filamu kuwa na makosa kwenye tafsiri zake, changamoto ya utamaduni, filamu kwenda kwa kasi, mtazamo hasi wa wanafunzi na changamoto ya umeme. Utafiti huu umependekeza kwamba vituo vinavyofundisha Kiswahili kwa wageni viboreshe mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji.

Maneno Muhimu: *Tafsiri, Filamu za Kibongo, Msamiati, Kiswahili na Wageni*

Utangulizi na Mapitio ya Maandishi

Watu hujifunza lugha kwa lengo la kuvasiliana kwa ufasaha wakitumia lugha hiyo katika mazingira mbalimbali, yaani kutoa na kupokea habari (Canele na Swain, 1980). Ili kulifikia lengo hilo, msamiati wa kutosha wa lugha husika (lengwa) unahitajika. Hii ni kwa sababu msamiati ndicho kiini cha mawasiliano kwa kila lugha. Kadhalika, stadi kuu za lugha ambazo ni kusoma, kusikiliza, kuandika na kuzungumza hutegemea utambuzi wa msamiati wa lugha husika (Schimitt, 2000; Cameron, 2001). Kiwango cha msamiati wa lugha lengwa alichonacho mjifunzaji lugha ndicho hutabiri uwezekano wake wa kuelewa na kutumia lugha hiyo (Edge, 1993). Edge anaendelea kueleza kuwa uhaba wa msamiati wa lugha lengwa husababisha ugumu au kukatika kwa mawasiliano ya mjifunzaji katika lugha hiyo. Aidha, mjifunzaji wa lugha hawezi kujieleza vizuri kwa lugha ya mazungumzo au maandishi bila msamiati wa kutosha wa lugha lengwa. Kwa mantiki hiyo, ni muhimu kwa walimu wanaofundisha lugha za kigeni au kwa wageni kuzingatia kipengele hiki wanapofundisha darasani ili kuwawezesha wanafunzi wao kupata msamiati mwingi kwa ajili ya kuvasiliana kwa ufasaha. Ili kulifikia hili, matumizi ya nyenzo/zana zenyne kuchagiza uibuzi wa ingizo la msamiati ni jambo muhimu.

Ufundishaji wa msamiati darasani si jambo rahisi. Msamiati huwatatiza wanafunzi wengi wa lugha za kigeni (Meara, 1980). Hii ina maana kwamba wanafunzi wengi hushindwa kupata msamiati wa lugha husika kwa wakati. Hii inatokana na ukweli kwamba ujifunzaji wa msamiati hauhusishi kanuni zilizo wazi zinazomwongoza mjifunzaji kujifunza kipengele hiki kama ilivyo kwa vipengele vingine vya lugha. Ugumu mwingine wa kujifunza msamiati unatokana na neno moja kuakisi maana zaidi ya

¹ Kukamilika kwa shahada hiyo ni kutokana na ufadhlili wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki. Mchango wao tunautambua na kuuthamini sana.

moja (Oxford, 1990). Hashemi na Pourgharib (2014) wanaeleza kuwa tofauti na ujifunzaji wa sarufi ambayo huhusisha kanuni mbalimbali, msamiati ni kipengele kinachohitaji kukumbuka. Hivyo, matumizi ya mbinu na nyenzo zenyewe wa kuwapa wajifunzaji ingizo toshelevu na linaloelewaka kwa wepesi na kwa namna inayovutia ni muhimu ili kuwawezesha wajifunzaji kukumbuka msamiati wa Kiswahili.

Wataalamu mbalimbali wanapendekeza matumizi ya filamu zenyewe tafsiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa msamiati wa lugha za kigeni (taz. Zanon, 2006; Talavan, 2007; Raine, 2012; Hashemi na Pourgharib, 2014; Sadiku, 2018). Wataalamu hawa wanaeleza kuwa filamu zenyewe tafsiri ya kutoka lugha lengwa kwenda lugha chanzi ambapo mazungumzo yapo katika lugha lengwa na tafsiri yake kwa maandishi katika lugha chanzi ni faafu. Hii ni kutokana na umuhimu wake kama vile kuongeza motisha kwa mjifunzaji kuendelea kujifunza lugha; kuonesha matumizi ya lugha katika mazingira halisi na kuhusisha njia kuu za ujifunzaji wa msamiati ambazo ni kusikiliza na kusoma. Vilevile, filamu hurudiarudia maneno kwa kasi ya wazawa; huwasilisha ujumbe kwa lugha ya mazungumzo na kwa lugha ya ishara ambayo kwa uhakika humwezesha mjifunzaji kupata msamiati wa lugha anayojifunza kwa wepesi (Kunyun na Huayu, 2011).

Aidha, filamu zenyewe tafsiri huwasilisha ujumbe kwa njia tatu. Njia hizo ni picha, sauti na maandishi. Sauti na maandishi huunganishwa na tafsiri (Danan, 1992). Kwa mujibu wa Talavan (2007), wajifunzaji wa kiwango cha chini ambao mara nyingi hushindwa kuelewa maneno mbalimbali yanayotumika kwenye filamu hupata fursa ya kuelewa maneno hayo kupitia filamu zenyewe tafsiri. Talavan (2007) anaendelea kueleza kuwa tafsiri hiyo pia huwasaidia wajifunzaji wa ngazi ya juu kufahamu msamiati mpya na ule usio wa kawaida ambao vinginevyo usingefahamika kwa wanafunzi bila usaidizi wa tafsiri. Hivyo basi, mwanafunzi hupata msamiati huo kwa kusikiliza mazungumzo ya waigizaji, kusoma maandishi katika kiwambo na kuona matumizi ya msamiati huo katika miktadha halisi mbalimbali. Njia hizo kwa pamoja humwezesha mjifunzaji kuhifadhi msamiati aliofundishwa darasani na pia kuweza kuutumia baadaye kwa ufasaha katika mawasiliano yake ya kila siku. Kama anavyosema Zhang (2009), wanafunzi wanapendelea kujifunza msamiati kwa kutumia nyenzo zinazohusisha kuona na kusikia kuliko matumizi ya mbinu za kimapokeo kama chaki na ubao. Licha ya umuhimu huo, utafiti huu mdogo unachunguza changamoto zinazoathiri matumizi ya filamu za Kibongo zenyewe tafsiri katika ufundishaji wa msamiati wa Kiswahili kwa wageni nchini Tanzania.

Nadharia ya Ujifunzaji kwa Media Anuwai

Nadharia hii iliasisiwa na Mayer (1997) na kuendelezwa tena na Mayer (2009). Nadharia hii inaeleza kuwa akili ya mwanadamu huchakata taarifa kwa ufanisi zaidi kipitia mifumo miwili ya ufahamu ambayo ni kuona na kusikia. Mayer anaeleza kuwa akili ya mwanadamu ina uwezo mdogo wa kuchakata taarifa. Ili kuwezesha taarifa kuchakatwa vizuri na kwa urahisi zaidi, ni vyema mifumo ya kuona na kusikia ikamilishane. Hii ni kwa sababu kujifunza ni mchakato amilifu wa kuchuja, kuchagua, kupanga na kuunganisha taarifa. Filamu kama nyenzo inayohusisha uwasilishaji wa taarifa kipitia kusikia na kuona, ina uwezo mkubwa wa kuwawezesha wajifunzaji kuchakata taarifa kwa ufanisi zaidi.

Mayer anaeleza kuwa ujifunzaji bora hujitokeza zaidi pale watu wanapotumia picha na maneno kwa pamoja kuliko kutumia maneno peke yake. Maneno yanaweza kuwa katika sauti, maandishi au sauti na maandishi kwa pamoja. Vilevile, picha zinaweza kuwa katika mfumo wa picha zilizopigwa kwa kutumia kamera, michoro, au video. Hii ni kwa sababu binadamu ana mifumo miwili ya kuchakata taarifa ambayo ni kuona na kusikia; umbo la picha na umbo la usemi. Hivyo, nadharia hii inasisitiza matumizi ya mifumo zaidi ya mmoja, yaani sauti, picha na maandishi kila mwalimu anapofundisha kwani ndiyo huchagiza uchakataji wa taarifa kwa kiasi kikubwa kuliko kutumia mfumo mmoja. Mifumo miwili au zaidi hukamilishana ili kuongeza uchakataji wa taarifa na uelewa wa mjifunzaji. Kwa mantiki hiyo, filamu za Kibongo zenyewe tafsiri ambazo huwasilisha taarifa kipitia sauti, picha na tafsiri kwa maandishi ni faafu katika kumwezesha mjifunzaji kupata msamiati wa Kiswahili kwa wepesi ikilinganishwa na kusoma vitabu peke yake.

Nadharia hii ina kanuni kumi na mbili. Kanuni ya ushikamano/uvwiano, kuashiria, upungufu, mshikamano wa nafasi, mshikamano wa muda, kutenganisha, mafunzo ya awali, tabia/utaratibu, kujifunza kwa media anuwai, kubinafsisha, sauti na kanuni ya picha. Katika kueleza changamoto zinazoathiri matumizi ya filamu za Kibongo zenye tafsiri, mawazo ya nadharia hii pamoja na kanuni tatu kama zinavyoolezwa moja baada ya nyingine kwenye aya zinazofuata, zimetumika.

Kanuni ya ushikamano/uvwiano. Kanuni hii inapendekeza kuepuka matumizi ya media yenyen maneno, sauti na picha ambavyo havihuksiani moja kwa moja na kile kinachotarajiwa kufundishwa. Hii ina maana kuwa ujifunzaji unatokea kwa ufanisi zaidi kupitia yale maarifa yanayoendana na mada husika ambayo mwanafunzi anahitaji kwa wakati huo. Hivyo, mwalimu hana budi kuonesha tu kipengele kidogo cha filamu chenye maudhui muhimu kuliko kuonesha filamu nzima ndani ya muda wa kipindi chake. Kanuni ya mshikamano wa muda. Kanuni hii inaeleza kuwa ujifunzaji unatokea kwa ufanisi zaidi iwapo maneno na taswira/picha vinatokea kwa wakati mmoja bila kupishana. Hii ina maana kwamba sauti, vitendo na maandishi vyenye maana sawa vitokee kwenye kiwambo kwa wakati mmoja pasipo kupishana.

Kanuni ya kujifunza kwa media anuwai. Kanuni hii inaeleza kuwa watu hujifunza kwa ufanisi zaidi kupitia maneno na picha kuliko maneno peke yake. Maneno yanaweza kuwa kwa sauti au maandishi au vyote kwa pamoja. Kanuni hii ndiyo msingi wa kanuni zote, yaani inasisitiza kuwa ujifunzaji unatokea kwa ufanisi zaidi kupitia media mbalimbali kuliko kutumia media moja. Kanuni hii ina maana kwamba mwalimu atumie nyenzo zenye uwezo wa kuwasilisha maarifa kwa mifumo miwili au zaidi kila anapofundisha ili kuwawezesha wajifunzaji kujifunza kwa ufanisi zaidi. Kanuni hii inaunga mkono matumizi ya filamu za Kibongo zenye tafsiri katika uwasilishaji wa somo. Kwa kuwa kanuni hii inasisitiza kuwa matumizi ya nyenzo kama filamu ndiyo huchagiza ujifunzaji kwa ufanisi zaidi, kutumika kwa uchache au kutotumika kabisa kwa filamu za Kibongo zenye tafsiri kunawenza kuwachelewesha wajifunzaji katika kupata umilisi wa Kiswahili kwa wakati.

Changamoto Zinazoathiri Matumizi ya Filamu za Kibongo zenye Tafsiri katika Ufundishaji wa Msamiati wa Kiswahili kwa Wageni Nchini Tanzania

Sehemu hii inawasilisha data zinazoonesha changamoto zinazoathiri matumizi ya filamu za Kibongo zenye tafsiri katika ufundishaji wa msamiati wa Kiswahili kwa wageni. Changamoto hizo ni kama zifuatazo:

Ukosefu wa Vitendeakazi

Kwa kuchunguza data za utafiti huu, inabainika kuwa matumizi ya filamu za Kibongo zenye tafsiri huathiriwa na uhaba wa vitendeakazi. Kwa mujibu wa BAKITA (2017), kitendeakazi ni zana au kifaa cha kufanya kazi. Kulingana na utafiti huu, vitendeakazi ni vifaa kama kompyuta, projekta, kiwambo, spika na vifaa vingine. Walimu walieleza kuwa wana uhaba wa vifaa vinavyoweza kuonesha filamu kwa wanafunzi wote kwa uwazi pale ambapo darasa linakuwa kubwa. Mathalani, baadhi ya walimu walikuwa na haya ya kusema:

Dondoo A:

...matumizi ya filamu darasani yanamhitaji mwalimu kutumia vifaa vya kiteknolojia mbalimbali... Wakati mwengine unaweza kukosa vifaa vya kutumia kuonesha filamu hasa darasa likiwa kubwa. Ikiwa kuna wanafunzi wengi kwenye darasa lako unahitaji kutumia projekta au kiwambo kikubwa ili kile kinachooneshwa kiwe wazi kwa wanafunzi wote. ...inakuwa vigumu kutumia filamu kwenye darasa kubwa kwa kutumia kompyuta pakatwa na mara nyingi huwa tunatumia filamu ikiwa darasa lina wanafunzi wachache kwa sababu hapo ndipo tunaweza kutumia kompyuta zetu tofauti na darasa likiwa kubwa....

Dondoo B:

.... unapotumia zana au filamu yoyote darasani kwa ajili ya kufundishia, unapaswa kuhakikisha kuwa kila kinachotendeka mle kwenye filamu kinaonekana vizuri, yaani picha na maneno yale vionekane vizuri na sauti ile iwe inasikika kwa wanafunzi wote. Hii inahitaji vifaa vyenye uwezo wa kufanya hivyo kama projekta, kiwambo kikubwa ambavyo kwa sasa havipo.... Tunajitahidi kutumia kompyuta zetu lakini hii inawezekana pale tu darasa likiwa na wanafunzi wachache....

Chanzo: Data za Utafiti (2022)

Madondoo A na B yanadhihirisha kwamba walimu wana uhaba wa vitendeakazi. Walieleza kuwa wanakosa vitendeakazi kama viwambo vikubwa na projekta vyenye uwezo wa kuwasilisha maarifa kwenye filamu kwa uwazi pale ambapo darasa ni kubwa. Walimu wanajitahidi kutumia kompyuta zao pale tu darasa likiwa na wanafunzi wachache. Hii ina maana kwamba inakuwa vigumu kwa mwalimu kutumia filamu kwenye darasa lake akiwa na wanafunzi wengi kwenye darasa hilo. Hii ni kwa sababu, darasa likiwa kubwa, wanafunzi hawataweza kuona vizuri kile kinachotendeka kwenye filamu akitumia kompyuta pakatwa. Hii ina maana kwamba matumizi ya filamu za Kibongo zenyetafsiri darasani yanahitaji vifaa vyenye uwezo wa kuonesha filamu kwa uwazi kwa wanafunzi wote hasa darasa likiwa kubwa.

Maeleo haya yanaungwa mkono na matokeo kutoka ushuhudiaji. Kati ya vituo vitatu vilivyotembelewa kwa ajili ya kukusanya data za utafiti huu, kituo kimoja tu kilibainika kuwa na projekta na viwambo vikubwa kwenye zaidi ya madarasa mawili japokuwa si katika kila darasa. Vile vituo viwili vingine havikuwa na viwambo vikubwa kwenye madarasa yao. Mwalimu katika kituo kimoja kisicho na viwambo vikubwa kwenye madarasa yao alifundisha kwa kutumia kompyuta pakatwa yake na hii iliwezekana kwa kuwa kulikuwa na wanafunzi wachache kwenye darasa lake wakati huo. Hali hii inadhihirisha kuwa matumizi ya filamu za Kibongo zenyetafsiri katika ufundishaji wa msamiati wa Kiswahili kwa wageni huathiriwa na changamoto ya ukosefu wa vitendeakazi.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Ujifunzaji kwa Media Anuwai ya Mayer (2009), media inayofaa kutumika darasani kufundishia ni ile ambayo inawawezesha wajifunzaji kuona na kusikia kila kitu kinachowasilishwa kwa uwazi. Hii ni kwa ajili ya kuwawezesha wajifunzaji wote kuona na kusikia kila kinachoendelea kwenye filamu husika ili waweze kujifunza kwa ufanisi zaidi. Uhaba wa vifaa kama viwambo vikubwa na projekta hukwamisha matumizi ya filamu za Kibongo zenyetafsiri pale ambapo darasa linakuwa kubwa. Hii ni kwa sababu bila vifaa vyenye uwezo wa kuwasilisha kwa uwazi maarifa yaliyopo kwenye filamu kwa wanafunzi wote, mwalimu hawezi kutumia filamu kwenye darasa lake.

Filamu Kuchukua Muda Mwingi wa Kipindi

Walimu walieleza kuwa filamu huchukua muda mrefu na kuwanyima nafasi ya kufanya majadiliano kuhusu kile ambacho kimetazamwa, jambo ambalo linasababisha kutofikiwa kwa malengo ya somo. Madondoo CH na D yanawakilisha mawazo ya watoataarifa hao.

Dondoo CH:

...filamu inachukuwa muda mwangi wa kipindi ikitumika darasani. Muda mrefu unahitajika kutazama filamu kwa sababu wanafunzi wanahitaji watazame filamu kwa zaidi ya mara moja ili waweze kuelewa vizuri kile kinachowasilishwa mle. Filamu ikirudiwa kutazamwa, unakuta karibu muda wote wa kipindi umeisha na hapo bado hamjachambua maudhui yake na kwa kuwa filamu inahusisha mambo mengi, mnajikuta mnahitaji kujadili vitu vingi wakati muda hauwawezeshi....

Dondoo D:

...matumizi ya filamu darasani yanahitaji muda wa kutosha lakini kumbuka sisi tunafundisha kwa kufuata ratiba zilizoandaliwa na wakubwa wetu na kila kipindi kina muda wake maalumu... Baadhi ya filamu ni ndefu kiasi kwamba masaa yanahitajika ili kuzitazama hadi mwisho....unajikuta muda wako wa kipindi umekwisha wakati hamjamaliza mambo ya msingi uliyokusudia kufundisha kwenye kipindi hicho....

Chanzo: Data za Utafiti (2022)

Kwa kurejelea maelezo ya walimu katika madondoo CH na D hapo juu, imebainika kuwa filamu huchukua muda mwiningi wa kipindi, jambo ambalo linawanyima walimu nafasi ya kufikia malengo yao. Walimu walisema kuwa wanaonesha filamu zaidi ya mara moja ili kuwawezesha wanafunzi kuelewa vizuri kile kinachowasilishwa kwenye filamu. Vilevile, walimu walieleza kuwa baadhi ya filamu ni ndefu kiasi kwamba zinahitaji muda mrefu kuzitazama. Hivyo, walimu wanajikuta muda wa kipindi uliopangwa umeisha kabla ya kufanya majadiliano kuhusu mambo muhimu na hivyo kushindwa kufikia malengo ya somo.

Maelezo haya yanashadidiwa na matokeo ya ushuhudiaji ambapo baadhi ya walimu walionesha filamu kwa zaidi ya dakika arobaini. Hivyo, muda mchache ulibaki kwa ajili ya majadiliano, jambo ambalo lisababisha baadhi ya maneno mapya yaliyotajwa na wanafunzi kutotolewa ufanuzi. Hata hivyo, matokeo haya yanaonesha kuwa baadhi ya walimu hawana ujuzi wa kutosha kuhusu namna ya kutumia filamu katika madarasa yao. Kwa hakika, muda wa saa mbili uliopangwa kwa kila kipindi unaweza kutosha kutumia filamu darasani na kufikia malengo ya somo. Walimu wanahitaji tu kuboresha namna wanavyotumia filamu kufundishia ili waweze kutimiza malengo ya somo. Kwa mfano, wakati wa kipindi mwalimu anaweza kuonesha ile sehemu ndogo tu ya filamu inayobeba maarifa muhimu yanayohitajika kwa wakati huo badala ya kuonesha filamu nzima. Hii inasaidia kuokoa muda na kumwezesha mwalimu kufikia malengo yake ndani ya muda wa kipindi kama ulivyopangwa.

Wataalamu kama Massi na Blazquez (2012) wanapendekeza matumizi ya filamu fupi darasani, yaani wanafunzi wasitazamishwe filamu kwa zaidi ya dakika kumi na tano. Kwa mujibu wa Massi na Blazquez (2012), filamu ikiwa ndefu inawachosha wajifunzaji na kuondoa umakini wao na kuwa kikwazo katika ujifunzaji. Hivyo, wanapendekeza matumizi ya filamu fupi ili kuwawezesha wajifunzaji kuwa makini zaidi. Kwa mantiki hiyo, mwalimu anashauriwa kuonesha kile kipengele tu cha filamu kinachobeba maudhui yanayohitajika kwa wakati huo kuliko kuonesha filamu nzima wakati wa kipindi. Vilevile, kanuni ya ushikamano/ uwiano ya Nadharia ya Ujifunzaji kwa Media Anuwai ya Mayer (2009) inasisitiza kuonesha ile sehemu ndogo ya filamu yenyeye yale maarifa tu ya msingi yanayoendana na mada husika. Hii inasaidia kuokoa muda wa kipindi na kumwezesha mwalimu kufikia malengo ya somo.

Filamu Kuwa na Makosa katika Tafsiri Zake

Changamoto nyingine inayoathiri matumizi ya filamu za Kibongo zenyeye tafsiri katika ufundishaji wa msamiati wa Kiswahili kwa wageni, ni filamu kuwa na makosa kwenye tafsiri zake. Walimu walieleza kuwa, tafsiri inayojitokeza kwenye filamu nyingi za Kibongo inapotoshwa ujumbe unaokusudiwa na waigizaji kwenye filamu husika. Kwa mujibu wa Newmark (1988), makosa katika tafsiri ni kutafsiri neno, kirai au sentensi kwa namna ambayo haileti maana ileile kama inavyowasilishwa kwenye lugha chanzi. Maelezo yao ni kama yanavyowakilishwa na baadhi ya maoni ya walimu katika madondoo E na F.

Dondoo E:

...filamu nyingi za Kibongo zina makosa kwenye tafsiri ile iliyofanyika.unakuta kile kinachosemwa kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa ile tafsiri iliyofanyika mle unakuta ilikosewa.... si vizuri kupeleka filamu ya namna hiyo darasani kwa wanafunzi hata kama msisitizo unawekwa kwenye kuona na kusikia mazungumzo lakini na yale maandishi yanatakiwa kuendana na kile kinachosemwa mle kwenye filamu kwa sababu hiyo tafsiri

yenyewe inawasaidia wanafunzi kuelewa kwa undani kile kinachoendelea mle kwenye filamu....

Dondoo F:

...sababu mojawapo ya kutumia filamu zenyet tafsiri ni kumrahisishia mjifunzaji kuelewa kwa undani kile kinachofanyika kwenye filamu ili aweze kukihusianisha na ile lugha anayojifunza.... Tafsiri hiyo inapokosewa inamkanganya na kumpoteza mwanafunzi badala ya kumsaidia na hii inakuwa changamoto kubwa kwa sababu inakwamisha ujifunzaji wa mwanafunzi....

Chanzo: Data za Utafiti (2022)

Data katika madondoo E na F zinadhihirisha kuwa filamu za Kibongo zina makosa kwenye tafsiri zake. Walimu walieleza kuwa tafsiri inayopatikana kwenye filamu nyingi za Kibongo ilikosewa ambapo ile tafsiri iliyofanyika haileti maana sawa na lugha inayozungumzwa na waigizaji kwenye filamu. Hii ina maana kwamba tafsiri iliyofanyika kwenye filamu inapotosha maana ya ujumbe unaozungumzwa na waigizaji. Walimu walieleza kuwa, tafsiri hiyo inapokosewa, huwakanganya na kuwapoteza wanafunzi badala ya kuwasaidia. Hivyo, kukwamisha ujifunzaji wao wa Kiswahili.

Hoja kwamba filamu za Kibongo zinahusisha makosa kwenye tafsiri zake inaungwa mkono na Ngunguti (2011) ambaye alifanya utafiti kuhusu makosa ya tafsiri yanayojitokeza kwenye filamu za Kibongo. Hata kama Ngunguti hakuchunguza filamu za Kibongo zenyet tafsiri katika muktadha wa ufundishaji na ujifunzaji, alibaini kuwa filamu za Kibongo zinahusisha makosa ya kutafsiri. Baadhi ya makosa aliyoyabaini ni pamoja na makosa ya kimofolojia, makosa ya kisintaksia, makosa ya kiutamaduni na makosa mengine. Hivyo, makosa hayo hukwamisha ujifunzaji wa mwanafunzi.

Hata hivyo, katika hali halisi, ni vigumu kupata tafsiri ambayo haina makosa kwa asilimia mia (100%) kutokana na tofauti za kiutamaduni kati ya lugha moja na nyingine. Kwa mantiki hiyo, mwalimu anashauriwa kutumia muda wake kuchagua filamu ambayo angalau makosa yake hayaleti athari kubwa kwenye maana iliyokusudiwa na waigizaji kwenye filamu husika.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Ujifunzaji kwa Media Anuwai ya Mayer (2009), ufanisi katika ujifunzaji unatokea zaidi ikiwa kuna uwiano wa maarifa/maana kati ya lugha ya mazungumzo na lugha ya maandishi. Hii ina maana kwamba makosa ya kutafsiri yanayojitokeza kwenye filamu za Kibongo hukwamisha ujifunzaji. Hivyo, kuwafanya walimu walio wengi kukwepa filamu hizo wanapokuwa wanafundisha Kiswahili kwa wageni.

Filamu Kwenda kwa Kasi

Watoataarifa wa utafiti huu walieleza kuwa filamu za Kibongo zenyet tafsiri huenda kwa kasi ikilinganishwa na uzoefu wa wanafunzi wao katika lugha ya Kiswahili. Walimu walisema kuwa wajifunzaji wa ngazi ya chini na kati hupata shida kuelewa ile lugha inayotumika kwenye filamu kwa sababu ya kasi inayotumiwa na waigizaji. Baadhi ya watoataarifa hao walikuwa na haya ya kusema:

Dondoo G:

...filamu nyingi za Kibongo zinaenda tuseme kwa kasi sana kulingana na wanafunzi ninaowafundisha. Unakuta yale mazungumzo yanakimbia sana na mwanafunzi anapata shida kuelewa. ...filamu hizi ziliandaliwa na wazawa wa Kiswahili kwa ajili ya wenyeji wa Kiswahili. Hivyo, zinapotumika darasani kama nyenzo ya kufundishia kwa mwanafunzi anayejifunza Kiswahili kama lugha yake ya kigeni, mara nyingi mwanafunzi huyo anapata wakati mgumu kuelewa kile kinachozungumzwa hasa wale wa ngazi ya chini...

Dondoo H:

...filamu nyingi huwa kwa kasi kana kwamba mjifunzaji wa lugha ya kigeni anashindwa kufuatilia yale mazungumzo. ...filamu hizi hazikutayarishwa kwa ajili ya kufundishia Kiswahili kwa wageni na filamu nyingi waigizaji wanaongea kwa haraka sana. ...wajifunzaji wanashindwa kusikia vizuri yale maneno ya Kiswahili yanayotumiwa kwenye filamu ambayo ni msingi wa kujifunza msamiati.

Chanzo: Data za Utafiti (2022)

Madondoo G na H ni maelezo ya walimu kuhusu changamoto ya filamu kwenda kwa kasi. Walimu walieleza kuwa filamu nyingi za Kibongo zinakimbia sana ukilinganisha na uzoefu wa lugha walionao wajifunzaji wao. Walimu walieleza kuwa filamu hizi ziliandaliwa na wazawa wa Kiswahili kwa ajili ya wenyeji wa Kiswahili. Hivyo, hazikutengenezwa/kutayarishwa kwa ajili ya kufundishia Kiswahili kwa wageni. Walimu waliendelea kueleza kuwa, kutokana na kasi ya filamu hizo, inakuwa vigumu kwa mjifunzaji wa ngazi ya chini anayejifunza Kiswahili kusikia na kuelewa mazungumzo ya waigizaji kwenye filamu. Hivyo, inakuwa vigumu kwake kujifunza msamiati wa Kiswahili kupitia filamu hizo.

Hoja kwamba filamu zinakwenda kwa kasi sana ilishawahi kudokezwa na Ramli (2019) katika utafiti wake kuhusu matumizi ya filamu zenye tafsiri katika ufundishaji wa lugha za kigeni. Ramli aligundua kwamba wajifunzaji walikumbana na changamoto ya filamu kwenda kwa kasi sana japokuwa yeye alishughulikia ufundishaji wa matamshi. Filamu kwenda kwa kasi husababisha athari hasi katika ujifunzaji. Picha na sauti vinapokwenda kwa haraka sana, huwfanya wajifunzaji washindwe kusikia na kuelewa kile kinachowasilishwa kwenye filamu. Hii ni kwa sababu wajifunzaji hao wanakuwa hawana uzoefu na lugha hiyo. Ndiyo maana filamu huonekana kama inakwenda kwa haraka sana ikilinganishwa na kiwango chao cha ujifunzaji.

Hata hivyo, kwa uelewa wa watafiti, changamoto hii inaweza kutokea kutokana na tajriba ya mwalimu katika kutumia mbinu na zana za kiteknolojia. Hii ni kwa sababu kupitia teknolojia, kuna uwezekano wa kupunguza au kuongeza kasi ya filamu kulingana na namna mtumiaji anavyotaka yeye mwenyewe. Hivyo, mwalimu anaweza kuongeza au kupunguza kasi ya filamu ili iendane na kiwango cha wanafunzi wake ili kuwawezesha kusikia kila neno linalosemwa na waigizaji. Hivyo, hoja kwamba filamu zinaenda kwa kasi sana kama ilivyoelezwa na walimu inaonesha kuwa baadhi ya walimu hawana maarifa ya kutosha kuhusu matumizi ya vifaa vya kiteknolojia. Aidha, Nadharia ya Ujifunzaji kwa Media Anuwai ya Mayer (2009) inaeleza kuwa media inayofaa kutumika darasani ni ile inayowawezesha wajifunzaji kusikia na kuona maarifa yote yanayowasilishwa kwa uwazi. Hivyo, filamu inapokwenda kwa kasi sana na kumzuia mwanafunzi kupata yale maarifa yanayowasilishwa kwenye filamu husika, hukwamisha ujifunzaji kwa mjifunzaji kwa sababu anakuwa hana uwezo wa kuelewa kile kinachowasilishwa kwenye filamu hiyo.

Changamoto ya Utamaduni

Changamoto nyingine inayoathiri matumizi ya filamu za Kibongo zenye tafsiri katika ufundishaji wa msamiati wa Kiswahili kwa wageni, kwa mujibu wa data za utafiti huu, ni changamoto ya utamaduni. Watoataarifa walisema kuwa filamu za Kibongo zinahusisha ubaguzi utokanao na mambo ya utamaduni kama vile vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia ambapo hasa wanawake hunyanyaswa na wanaume zao. Vitendo kama hivyo huibua hisia kwa wajifunzaji ambazo zinaathiri ujifunzaji wao. Maelezo ya baadhi ya watoataarifa wenyewe yanadhihirika katika madondoo I na J.

Dondoo I:

...changamoto kubwa ambazo zinatokea sana ni changamoto za kiutamaduni....mara nyingi filamu huwa zinaleta hisia kwa wanafunzi na hisia hizo zinaweza kuwa nzuri au mbaya. Kwa mfano, filamu ya Amelia....yule mama ameoneewa yaani amenyanyaswa sana na hii mara nyingi inaweza kusababisha hisia za mtu zikamwondoza katika somo....unaweza kuweka filamu halifu mwisho unakuta karibu wanafunzi wote wanalia....

Dondoo J:

...filamu nyingi za Kibongo zinahusisha lugha na vitendo vya ubaguzi yaani zinahusisha matendo ambayo hayaheshimu mambo ya usawa wa kijinsia. Baadhi ya filamu zinaonesha matendo ya unyanyasaji wa kijinsia yanayomkandamiza mwanamke.... mwanafunzi mwenye mtazamo tofauti na ubaguzi wa kijinsia awe mwanaume au mwanamke atachukia filamu hiyo jambo ambalo linaathiri ujifunzaji wake....

Chanzo: Data za Utafiti (2022)

Kwa mujibu wa madondoo I na J hapo juu, baadhi ya filamu za Kibongo zenyе tafsiri zinahusisha mambo ya kiutamaduni ambayo yana athari hasi katika ujifunzaji. Walimu walieleza kuwa filamu zinahusisha vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia ambapo wanawake hasa ndiyo hunyanyaswa na wanaume zao. Filamu za namna hiyo huwaondoa wanafunzi kwenye hali ya kujifunza na kuwajengea chuki. Kwa mfano, filamu inaweza kuwafanya wanafunzi walie ndani ya kipindi, jambo ambalo ni kikwazo cha kujifunza. Mathalani, wale wenye mtazamo hasi kuhusu masuala ya kijinsia wanaweza kuathiriwa sana. Kama inavyoolezwa na Nadharia ya Ujifunzaji kwa Media Anuwai ya Mayer (2009), ujifunzaji hutokea kwa ufanisi zaidi kuititia media/zana inayomvutia mwanafunzi. Hivyo, filamu zinazohusisha mambo ya unyanyasaji kama vile wa kijinsia zinakuwa kikwazo katika ujifunzaji. Hii ni kwa sababu filamu hizo huwajengea chuki wajifunzaji. Hivyo, changamoto ya utamaduni hukwamisha matumizi ya filamu za Kibongo zenyе tafsiri katika ufundishaji wa msamiati wa Kiswahili kwa wageni.

Mtazamo Hasi wa Wanafunzi kuhusu Kutazama Filamu

Watoataarifa walipoulizwa changamoto zinazoathiri matumizi ya filamu za Kibongo zenyе tafsiri katika ufundishaji wa msamiati wa Kiswahili kwa wageni, walitaja mtazamo hasi wa wanafunzi. Walimu walieleza kuwa baadhi ya wanafunzi huzichukulia filamu kama uongo mtupu unaoigizwa. Wanafunzi wenye mtazamo kama huo juu ya filamu hupata shida iwapo filamu itatumika kufundishia darasani kwa sababu hawawezi kuwa makini kwenye kile kinachooneshwa kwenye filamu hiyo. Hivyo, inakuwa vigumu kwa mwanafunzi mwenye mtazamo hasi kujifunza kuititia kutazama filamu. Maelezo ya baadhi ya watoataarifa katika madondoo K na L hapa chini yanadhihirisha hoja hiyo.

Dondoo K:

...kuna wanafunzi ambaо hawapendelei kutazama filamu maishani mwao. Mwanafunzi wa namna hiyo hupata shida kujifunza ikiwa filamu itatumika kama nyenzo ya kufundishia darasani...

Data L:

...baadhi ya wanafunzi hawapendi kutazama filamu kwa sababu wanadhani kuwa filamu ni uongo tu. Mwanafunzi mwenye mtazamo kama huo ni ngumu kujifunza kuititia filamu na hii inaathiri ujifunzaji wake iwapo filamu itatumika darasani kwa sababu hatakuwa makini kwenye kutazama kile kinachowasilishwa kwenye filamu husika....

Chanzo: Data za Utafiti (2022)

Kwa kuchunguza madondoo K na L hapo juu, tunaona kuwa kuna wanafunzi ambaо hawapendelei kutazama filamu kwenye maisha yao. Hii ni kwa sababu wanafunzi hao huchukulia filamu kama uongo mtupu. Walimu walieleza kuwa mtazamo hasi kama huo hupunguza umakini wa mjifunzaji wa kufuutilia filamu husika, jambo ambalo hukwamisha ujifunzaji wao. Wajifunzaji wanapokuwa na mtazamo hasi, umakini wao unaathirika na matokeo ya kutumia filamu husika yanakuwa hasi. Hivyo, utafiti huu umebaini kuwa mtazamo hasi wa wajifunzaji kuhusu kutazama filamu ni mojawapo ya changamoto zinazoathiri matumizi ya filamu za Kibongo zenyе tafsiri katika ufundishaji wa msamiati wa Kiswahili kwa wageni. Aidha, kulingana na Nadharia ya Ujifunzaji kwa Media Anuwai ya Mayer (2009), mwanafunzi anapaswa kuwa makini kwenye media inayotumiwa darasani ili aweze kuona na kusikia (picha na maneno) kwenye media kwa ajili ya kujifunza kwa ufanisi zaidi. Hivyo, mtazamo hasi juu ya filamu unajenga chuki kwa mjifunzaji ambayo ni kikwazo cha ujifunzaji.

Changamoto ya Umeme

Kulingana na data za utafiti huu, imebainika kwamba matumizi ya filamu za Kibongo zenyе tafsiri huathiriwa na changamoto ya umeme. Ilielezwa kuwa inakuwa vigumu kutumia filamu kwa vile umeme si wa uhakika. Akizungumzia hili, mtoataarifa mmoja alisema:

Dondoo M:

...umeme huwa hautabiriki, huwezi kujua utakatika saa ngapi au lini. Matumizi ya filamu darasani yanahitaji kutumia vifaa kama projekta, viwambo ambavyo utendakazi wake unategemea sana nguvu za umeme. ...unajikuta umejiandaa kutumia filamu kwenye kipindi chako lakini kufika darasani, unakuta umeme umekatika na wakati mwingine mnaweza kuwa katikati mwa onesho la filamu halafu umeme unakatika gafla na kwa bahati mbaya sisi hapa hatuna jenereta ambayo unaweza kusema kwamba utaitumia iwapo umeme umekatika...

Chanzo: Data za Utafiti (2022)

Dondoo M linabainisha kuwa umeme huwa hautabiriki lini utakatika kwani unaweza kukatika muda wowote iwe kabla au katikati mwa onesho la filamu darasani. Walimu walieleza kuwa matumizi ya filamu darasani yanahitaji vifaa kama projekta na viwambo ambavyo utendakazi wake unategemea nishati ya umeme. Hii ina maana kwamba ni vigumu kwa mwalimu kutumia filamu kwenye darasa lake bila umeme. Umeme ukikatika katikati au kabla ya kutazama filamu, mwalimu hawezu kufanikisha malengo ya somo hilo wakati huo. Vilevile, walimu walisema kuwa hawana jenereta ambayo wanaweza kutumia ikiwa umeme umekatika. Hivyo, inakuwa vigumu kwao kutumia filamu kufundishia pale darasa linapokuwa kubwa. Hii ni kwa sababu si rahisi kuonesha filamu kwa darasa kubwa kwa kutumia kompyuta pakatwa ambayo inaweza kutumika kwa muda fulani hata kama umeme umekatika.

Maelezo haya kutoka kwa mto mtoataarifa yalithibitishwa na ushuhudiaji ambapo kati ya vituo vitatu viliviyotembelewa, ni kituo kimoja tu ambacho kilikuwa na jenereta yenyewe uwezo wa kufanya kazi wakati wowote. Kituo kingine kilikuwa na jenereta lakini ilikuwa mbovu kwa muda unaozidi mwaka mzima kwa mujibu wa mtoataarifa. Hivyo, ni kama hawakuwa na jenereta. Kituo cha tatu hakikuwa na jenereta yoyote kwa mujibu wa watoataarifa. Hii inaonesha kwamba iwapo umeme utakatika kabla au katikati ya onesho la filamu darasani, ufundishaji unatatzika na malengo ya mwalimu ya somo hilo yanaweza kutofikiwa ipasavyo. Hivyo, utafiti huu umebaini kuwa kukatika kwa umeme kunakwamisha matumizi ya filamu za Kibongo zenyewe tafsiri katika ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni.

Hata hivyo, mwalimu anaweza kutumia kompyuta pakatwa yake kuonesha filamu kwa wajifunzaji hasa pale anapokuwa na wajifunzaji wachache kwenye darasa lake. Hii inaweza kumsaidia kutumia filamu hata bila kuwapo kwa umeme. Hii ni kwa sababu si lazima kutumia projekta na kiwambo kikubwa kila wakati mwalimu anapofundisha. Iwapo darasa ni dogo na mwalimu anahitaji kutumia filamu fulani, anaweza kutumia kompyuta pakatwa kuliko kutotumia filamu kabisa ili aweze kufikia malengo yake. Hii ni kwa sababu baadhi ya kompyuta pakatwa zina uwezo wa kuhifadhi moto kwa muda fulani. Changamoto hii ya kukatika kwa umeme itabaki iwapo darasa ni kubwa kwa sababu si rahisi kutumia kompyuta pakatwa ikiwa kuna wanafunzi wengi kwenye darasa.

Kama inavyoelezwa na Nadharia ya Ujifunzaji kwa Media Anuwai ya Mayer (2009), kupitia kanuni ya ujifunzaji kwa media anuwai, ufanisi katika ujifunzaji hutokeea kwa ufanisi zaidi kupitia matumizi ya media zaidi ya moja kwa maana ya picha na maneno kwa pamoja. Kukatika kwa umeme kunazuia matumizi ya nyenzo kama vile filamu zenyewe uwezo wa kuwasilisha maarifa kupitia kuona na kusikia (picha na maneno), jambo ambalo linaweza kusababisha kutofikiwa kwa malengo ya somo.

Hitimisho

Makala haya yameweka wazi changamoto mbalimbali zinazoathiri matumizi ya filamu za Kibongo zenyewe tafsiri katika ufundishaji wa msamiati wa Kiswahili kwa wageni. Changamoto hizo ni kama vile: ukosefu wa vitendeakazi, filamu kuchukua muda mwangi wa kipindi, filamu kuwa na makosa kwenye tafsiri zake, filamu kwenda kasi, changamoto za utamaduni, mtazamo hasi wa wanafunzi na changamoto ya umeme. Changamoto hizi zilikuwa hazijawekwa bayana kabla ya kufanyika kwa utafiti huu. Tafiti tangulizi kama utafiti wa Ramli (2019) ulidokeza changamoto moja tu ya kutumia filamu zenyewe tafsiri katika ufundishaji wa lugha za kigeni kwa ujumla. Changamoto iliyodokezwa na

Ramli ni filamu kwenda kwa kasi. Tofauti na changamoto hiyo, utafiti huu umebaini changamoto zingine kama zilivyobainishwa hapo juu.

Kutokana na umuhimu wa matumizi ya filamu katika kuchagiza ujifunzaji wa lugha kwa wageni, kupitia makala haya tunatoa mapendeleko yafuatayo: Kwamba, vituo vinavyofundisha Kiswahili kwa wageni viboreshe mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji. Mathalani, kuwe na vitendeakazi kama viwambo vikubwa, projekta, jenereta na vifaa vingine vyta kiteknolojia vinavyoweza kutumiwa kuonesha filamu kwa uwazi hata darasa likiwa kubwa. Hii itawawezesha walimu kutumia filamu za Kibongo zenyet tafsiri katika ufundishaji wa Kiswahili wakati wowote.

Aidha, tunapendekeza kuwa, wale wanaohusika na kutafsiri pamoja na kuingiza tafsiri kwenye filamu wawe wabobezi wa tafsiri. Hii itasidia kupunguza wingi wa makosa ya kutafsiri yanayojitokeza kwenye filamu za Kibongo zenyet tafsiri ili kuwawezesha walimu kutumia filamu hizi kwa ajili ya kufundishia Kiswahili kwa wageni.

Marejeleo

BAKITA. (2017). *Kamus Kuu ya Kiswahili (Toleo la 2)*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Cameron, L. (2001) *Teaching Languages to Young Learners*. Cambridge: Cambridge University Press.

Canele, M. na Swain, C. (1980). "Theoretical Basis of Communicative Approaches to Second Language Learning and Testing" *Applied Linguistics*, Juz.1 (1): 1 - 47 Inapatikana katika <http://applijji.oxfordjournal.org>. Ilisomwa tarehe 20. Oktoba. 2021.

Danan, M. (1992). "Reversed Subtitling and Dual Coding Theory: New Directions for Foreign Language Instruction". *Language Learning*, Juz. 42(4): 497-527. Inapatikana katika More-mobilenet-prefernetwaktye-aut acces point name-add-name TTCL –apn INTERNET save. Ilisomwa tarehe 12 Desemba 2021.

Edge, J. (1993). *Essentials of English Language Teaching*. Longman: New York.

Hashemi, H. na Pourgharib, B. (2014). "The Effect of Watching Standard Subtitled Audiovisual Materials on Improving Vocabulary Knowledge of Iranian EFL Learners". *International Journal of Basic Sciences & Applied Research*, Juz. 3: 227 – 252. Inapatikana katika <https://www.semanticscholar.org>. Ilisomwa tarehe 25 Januari 2022.

Kunyun, W. na Huayu, L. (2011). "Language Acquisition with the Help of Captions". *Studies in Literature and Language*, Juz. 3(3): 118 – 137. Inapatikana katika <https://dx.doi.org/10.3968/n>. Ilisomwa tarehe 17 Disemba 2021.

Massi, M.P. na Blazquez, B.A. (2012). "A Short Is Worthy a Thousand Films!". *Teaching English With Technology*, Juz. 12(3), 62-86. Inapatikana katika <http://www.tewtjournal.org>. Ilisomwa tarehe 15 Machi 2022.

Mayer, R.E. (1997). "Multimedia Learning: Are we asking the Right Questions? *Educational Psychologist*, Juz.32: 1-19. Inapatikana katika <https://doi.org/10.1207/s15326985ep3201-1>. Ilisomwa tarehe 27 Aprili 2022.

Mayer, R.E. (2009). *Multimedia Learning* (toleo la 2) New York: Cambridge: University Press.

Meara, P. (1980). "Vocabulary Acquisition: A Neglected Aspect of Language Learning". *Language Teaching and Linguistics*, Juz.13 (4): 221-246. Inapatikana katika <https://www.logistics.co.uk>. Ilisomwa tarehe 12 Novemba 2021.

Newmark, P. (1988). *A Textbook of Translation*. Landon: Prentice Hall.

Ngunguti, M.A. (2011). *Problems of Kiswahili-English Translation as Reflected in English Subtitles in Selected Tanzanian Kiswahili Movies*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Oxford, R.L. (1990). *Language Strategies. What Every Teacher should know?* Boston: Heinle and 323 Heinle.

Raine, P. (2012). *Incidental Learning of Vocabulary through Subtitled Authentic videos*. Birmingham: Birmingham University. Inapatikana katika: www.birmingham.ac.uk/Documents/collegeartslaw/cels/essays/matefltesdissertations/RAINE619605DISS.pdf. Ilisomwa tarehe 21 Februari 2022.

- Ramli, H.A. (2019). *The Use of "Inside Out" Movie's Subtitles to Improve Reading (A Case Study at Smk-Pp Saree)*. Banda Aceh: Universitas Islam Negeri Ar-Raniry. Inapatikana katika <https://core.ac.uk/download/pdf/293477462.pdf>. Ilisomwa tarehe 3 April 2022.
- Sadiku, A. (2018). “The Role of Subtitled Movies on Student’s Vocabulary Development”. *International Journal of Science and Basic Applied Research*, Juz. 42: 212 - 221.
Inapatikanakatika <https://gssrr.org/index.php/JournalOfBasicAndApplied/article/view/9407/4164>.
Ilisomwa 17 Juni 2022.
- Schimitt, N. (2000). *Vocabulary in Language Teaching*. Cambridge: Cambridge Universiy Press.
- Talava'n, N. (2007). “Leraning Vocabulary through Authentic Video and Subtitles” *TESOL-SPAIN Newsletter*, Juz. 31: 5-8. Inapatikana katika <http://www.researchgate.net>. Ilisomwa tarehe 10 Januari 2022.
- Zanon, N.T. (2006). “Using Subtitles to Enhance Foreign Language Learning”. *Porta Linguarum*, Juz. 6: 41-52. Inapatikana katika <http://hdl.handle.net/10481/30659>. Ilisomwa tarehe 25 Aprili 2022.
- Zhang, B. (2009). “Foreign Language Vocabulary Learning of Undergraduate English Majors in Western China: Perspective, Stratege Use and Vocabulary size”. *English Language Teaching*, Juz. 2: 178-185. Inapatikana katika <https://www.researchgate.net>. Ilisomwa tarehe 20 Agosti 2021.

